بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Jordan**

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

**Jumatano, 13 Rabi' II 1446 H** **16/10/2024 M** **Na: 1446 / 04**

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

## Mwaka Umepita, na Mauaji ya Kikatili ya Halaiki mjini Gaza Yanazidi na Kuenea. Je, Sio Wakati sasa kwa Ummah Kuwaondoa Watawala wake Waoga Ambao Wameshindwa Kuinusuru?! (Imetafsiriwa)

Licha ya mauaji ya mara kwa mara ambayo Palestina, na haswa Gaza, inapitia kila siku, yanayoongezeka hadi kufikia hatua ya kufa kwa moto na njaa, na mabomu yasiyokoma kwenye mikusanyiko ya watu waliohamishwa, kama inavyotokea leo kaskazini mwa Gaza, na zaidi ya mwaka mmoja baada ya ukatili wa majeshi ya Kiyahudi yenye silaha nzito, yakisaidiwa na nchi za kikoloni za Magharibi, watawala wa fedheha na uhaini wanaoizunguka Palestina na Gaza, walio umbali wa pua na mdomo, wanaendelea kutofanya lolote. Pamoja na kwamba Umma, wakiwemo watu wa Jordan, wanashuhudia yote hayo, bado utawala wa Jordan unaziba masikio kilio cha wanawake, watoto na wazee, na machozi ya wanaume wanyonge wanaopiga kelele kuomba msaada. Badala yake, unaendelea kucheza pamoja na mifumo ya kimataifa na ule inaoitwa uhalali wa kimataifa, ambao unaongozwa na Amerika, adui mkubwa wa Uislamu na Waislamu, ambayo inalitumia umbile la Kiyahudi kama chombo cha kuwafanyia unyama Waislamu na ardhi zao, ikifuata nyayo za Uingereza, mama wa usaliti na hadaa, na muundaji wa umbile la Kiyahudi, adui wa kihistoria wa Uislamu na Waislamu.

Mayahudi ni maadui wakubwa wa Uislamu na Waislamu, daima wakijitahidi kuwadhuru. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِّلَّذِينَ آمَنُواْ الْيَهُودَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُواْ]

**"Hakika utawakuta walio shadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walio amini ni Mayahudi na washirikina."** [Surat Al-Ma'ida:82].

Umbile hili ovu sio tu ni kadhia ya kiusalama, kijeshi, au ya kisiasa. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[لَن يَضُرُّوكُمْ إِلا أَذًى وَإِن يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الأَدْبَارَ ثُمَّ لاَ يُنصَرُونَ]

**"Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa."** [Surat Aal-i-Imran:111].

Inawezekana kulitokomeza na kuliondoa kwenye uso wa ardhi milele, kwa nguvu ya jeshi la Jordan pekee. Hii si ndoto au nadharia; wale wanaotilia shaka wanahitaji tu kuitazama Gaza, fahari, ambayo kwayo ilisimama kidete dhidi ya Mayahudi, ambao sura yao ilichanwa chanwa mbele ya ulimwengu, ikidhihirisha umbile lao halisi.

Sasa ni hakika kwa mtu yeyote mwenye macho kwamba watawala wa Kiarabu, hasa wale walio jirani na Palestina, wanafanya kazi na maadui wa Ummah ili kuhifadhi umbile la Kiyahudi. Wanashiriki hata katika vita vyake dhidi ya Waislamu wenzao. Matarajio ya mwisho ya watawala hawa ni dola ya kirongo ya Palestina chini ya udhibiti wa Mayahudi. Kwa zaidi ya mwaka mmoja, wamekuwa wakiomba sana katika majukwaa ya kimataifa kupunguza ongezeko la ghasia, wakihofia kupanuka kwa vita ambavyo vinaweza kusababisha kuanguka kwa tawala zao.

Kadhia ya Palestina, kwa msingi wake, ni kadhia ya Kiislamu, na kuliondoa umbile la Kiyahudi na kulifuta katika uwepo ni wajibu kwa Waislamu tangu kuasisiwa kwake. Baada ya mwaka wa mauaji, uharibifu, na uhamisho, wajibu huu umekuwa wa dharura zaidi.

**Enyi Wanajeshi katika Majeshi ya Waislamu na katika Jeshi la Jordan:** Ushujaa aliouonyesha shahidi, Mwenyezi Mungu akipenda, Maher Al-Jazi, ambaye alitenda peke yake, amelitukuza jina lake katika historia ya mashujaa watukufu, duniani na akhera, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Vitendo vyake vimetia fahari kwa watu wa Jordan na Umma mzima wa Kiislamu. Je, hamtashindana katika ushujaa huo na kuharakisha kutimiza faradhi ya Mola wenu kwa kupigana na adui yenu? Je, hamtatikisa udhaifu na utiifu kwa watawala wenu wanaokupelekaeni kwenye maangamivu, kuhakikisha kwamba hamburuzwi kwenye kumbukumbu za aibu na fedheha pamoja nao?

**Enyi watu wa Jordan, enyi Waislamu:** Wale wanaozuia jeshi lenu kulinda ardhi zenu, kuhifadhi mali zenu, na kukomboa ardhi zenu zinazokaliwa kwa mabavu, na wanaoijaza nchi kwa kambi za kijeshi za Marekani na Ulaya ili kulinda umbile la Kiyahudi, ni watawala wenu. Vita dhidi ya Gaza vimeweka wazi utiifu wao kwa makafiri na dori yao katika kuliwezesha umbile katili la Kiyahudi kwa kulilinda dhidi ya mashambulizi ya roketi. Watawala hawa ndio kikwazo ambacho lazima kiondolewe ili kuyawezesha majeshi yenu kuwanusuru Waislamu wa palestina. Msichoke kutaka kuhamasishwa kwa majeshi yenu ili muweze kuongoza njia ya kutokomeza umbile la Kiyahudi na dola za kikoloni zinazoliunga mkono.

**[قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ]**

**“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini”** [Surat At-Tawba:14]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Jordan**